NOA BONGO, JENGA MAISHA YAKO

# "Kabumbu Afrika - Ni zaidi ya mchezo!"

## KIPINDI CHA NNE: "Zaidi ya Mchuano"

**MWANDISHI: Chrispin Mwakideu**

**WAHARIRI: Andrea Schmidt, Thelma Mwadzaya**

- **ORODHA YA WAHUSIKA KIPINDI CHA NNE**
- **MSIMULIZI**

**SCENE ONE: AT AUNT LILY'S PLACE**

- Chedede (mume, 14)
- Safina (mke, 13)

**SCENE TWO: SOCCER CLINIC AT THE CITY STADIUM**

- Sauti za wavulana na wasichana (13+)
- Metogba (mume, 28)
- Wakasa (mwenyekiti uongozi wa soka, mume, 54)
- Komora (mume, 14)

**SCENE THREE: DUSTY PLAYGROUND IN TAMBARARE SLUMS**

- Chedede (mume, 14)
- Safina (mke, 13)

**SCENE FOUR: SOCCER CLINIC AT THE CITY STADIUM**

- Sauti za wasichana na wavulana (13+)
- Metogba (mume, 28)
- Komora (mume,14)
- Jonathan (mume,15)

**INTRO:**

**1.NARRATOR**: Salamu kemkem na karibuni katika kipindi chetu cha noa bongo, jenga maisha yako. Kama unajiunga nasi kwa mara ya kwanza, hii ni makala ya nne katika hadithi ya **"Kabumbu Afrika, ni zaidi ya mchezo!"** Katika makala iliyopita Chedede alipiga mpira na kulivunja dirisha la watu. Metogba, aliye mchezaji wa kulipwa, aliuelezea umuhimu wa kliniki ya soka. Kabla ya hapo, hakuliridhia ombi la mheshimiwa Makemba la kumteua mwanawe kabla ya mazoezi kuanza rasmi. Safina, msichana aliyetokea kijijini anyependa kucheza soka, aligundua kuwa shangazi yake sivyo alivyomdhania.Baki nasi hadi tamati katika makala ya leo ya **"Zaidi ya Mchuano"** tunaanza na Chedede aliyejawa na hofu baada ya kulivunja dirisha la kioo cha gari la watu….

**SCENE ONE: AT AUNT LILY'S PLACE**

**2. SFX: BROKEN GLASS SHATTERING ON THE FLOOR**

**3.** **SAFINA: (Screams out of fear)** Nisaidieni jamani!!! Shangazi Lily! Wezi! wezi!, wuuuuiiiii!

**4.** **SAFINA: (scared stiff)** Ni nani? Unataka nini kutoka kwangu? Ala! Kumbe ni mpira, lazima iwe mtu ameurusha huku kimakosa. Lo! Sasa nitamueleza nini shangazi Lily akirudi? Lazima niuhifadhi huu mpira kama ushahidi.

**5.** **SFX: FOOTSTEPS ON BROKEN GLASS**

**6.** **SAFINA: (Talking to self)** Lazima nijihadhari nisijikate.Salama nina viatu... sawa sasa ngoja nijue ni nani. **(Shouts)** Wewe! Wewe ndiye uliyevunja kioo cha dirisha letu?

**7.** **CHEDEDE: (from outside)** Hmm... ni mimi lakini si kupenda kwangu, tafadhali nirudishie mpira wangu.

**8.** **SAFINA: (Still loudly)** Eti nini? Samahani sana... lazima niuhifadhi huu mpira mpaka atakaporejea shangazi yangu. Nahitaji kumueleza kilichotokea.

**9.** **CHEDEDE: (threatening voice)** Sikiliza, msichana, mimi sitaki kuwa na matatizo na wewe. Nimekutaka radhi, sasa ni aidha unipe mpira au nitaingia mwenyewe kuuchukuwa…

**10.** **SAFINA:** Alaa, sasa unanitisha? **(sarcastic)** wacha nikupe habari basi... Kamwe sikuogopi. Mimi natokea kijijini na nimeshakutana na vijana wasiowajibika kama wewe kwa hivyo huu mpira huu hautoki hapa, hadi shangazi aje aamue mwenyewe.

**11.** **CHEDEDE: (takes a deep breath)** Nadhani namfahamu shangazi yako. Shangazi yako ni mkarimu… ataelewa. Sio mara ya kwanza hili limetokea. Kila wakati tunacheza mpira na kuvunja madirisha hapa. Linapotokea… baada ya hapo twaomba msamaha kisha yameisha.

**12.** **SAFINA:** Pengine ni hivyo, ila kwangu mimi ni mara ya kwanza kulishuhudia hilo. Hata hivyo, wewe ni mchezaji wa aina gani? Hukufahamu ulikokuwa unalenga?

**13.** **CHEDEDE:** Sasa naona wewe umevuka mipaka! Wewe ni msichana tu, wajua nini kuhusu kabumbu?

**14.** **SAFINA:** Hmm…sawa,tupigane mikwaju ya penalti tano kwa tano. Ukishinda ntakupa mpira wako na nikikushinda, mpira utakaa hapa umsubiri shangazi yangu aje.

**15.** **CHEDEDE: (laughs out loud)**

**16.** **SAFINA:** Bado sijamaliza. Tena wewe… kwa mdomo wako, utamueleza kilichotokea. Sawa?

**17.** **CHEDEDE:** Yaani hivi huu si utani?

**18.** **SAFINA:** Unaniona nikicheka? Mimi sifanyi masihara.

**19.** **CHEDEDE:** Kweli hujacheka, lakini nashangaa kwa nini tujisumbue? Nadhani ingekuwa rahisi zaidi ukinirejeshea mpira wangu na ujistiri badala ya kutaka tupigane penalti nikubandike mikwaju moto moto **(pause)** sawa, penalti... nasubiri.

**20.** **NARRATOR:** Dede alijua fikra kwamba itakuwa kama kumsukuma mlevi ila hakumfahamu mpinzani wake. Safina aliteremka chini mara moja wakacharazane mikwaju ya penalti na Chedede. Wakati huohuo, Metogba alikuwa anaanza siku yake ya kwanza katika kliniki ya soka, lakini alipofika, hakuamini alichokiona…

**SCENE TWO:SOCCER CLINIC AT THE CITY STADIUM**

**21.** **SFX: MIXED VOICES OF BOYS AND GIRLS 13 +**

**22.** **METOGBA: (worried)** Kwani kwaendelea nini? Tumekuwa hapa kwa muda wa saa zima na kuna vijana wangapi... **(counting)** moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane. Wachezaji wanane pekee ndio wamejitokeza?!

**23.** **WAKASA:** Hata si wanane, tuna wachezaji watano pekee. Wale watatu ni wasichana.

**24.** **METOGBA:** Ulisema wewe ndio nani mwenzangu vile?

**25.** **WAKASA:** Naitwa Sam Wakasa, mimi ndiye mwenyekiti wa shirikisho la soka nchini.

**26.** **METOGBA: (Not impressed)** Hmm... Kweli? Nashindwa kuelewa ulikipataje cheo hicho.

**27.** **WAKASA:** Umesema nini? Sikukupata vizuri?

**28.** **METOGBA:** Usitie shaka. **(serious tone)** Bwana Wakasa, siku hizi mambo yamegeuka. Katika kliniki hii ya soka,wasichana kamwe hawatabaguliwa. FIFA ni Shirikisho la Kimataifa la Kandanda. Herufi zake hizi zina maana nyengine pia F.I.F.A - Football-Is-For-All… yaani soka kwa wote. Hii inajumlisha wasichana, wavulana, wazee, matajiri, masikini, walemavu ilimradi unaweza kukimbia na kuupiga teke mpira. Soka inapaswa kufurahiwa na wote!

**29.** **WAKASA:** Lazima nikiri kuwa sijawahi kulifikiria hivyo. Hii ni kliniki yako mimi ni msaidizi tu. Tunaweza kuanza?

**30.** **METOGBA:** Ndio. Hatuna muda wa kupoteza.

**31.** **SFX: WHISTLE BLOWS/VOICES OF PLAYERS 13+CALM DOWN**

**32.** **METOGBA:** Hamjambo, karibuni nyote katika kliniki hii. Kwanza kabisa, ningependa tujitambulishe kwa majina. Ningependa kila mmoja wenu aseme jina lake, umri na dhamira ya kushiriki katika mazoezi haya. Kumbukeni! Msinidanganye. Ukinidanganya, halafu nijue ukweli, safari yako itakatikia hapo... mtu yeyote anaweza kuanza.

**33. KOMORA: (Hesitant)** Jina langu ni Komora… kusema kweli siujui umri wangu kamili. Nataka kujiunga na kiliniki hii kwa sababu nimeona hapa ndipo ndoto zangu zinaweza kutimia.

**34. METOGBA:** Komora, wewe unatokea wapi?

**35. KOMORA: (Still hesitant)** Sina makao kwa kweli naishi katika vichochoro vya Tambarare.

**36. METOGBA:** Sasa umepata makao, hii ni familia yako mpya, mwengine!

**37. NARRATOR:**Nadhani nakuona jinsi ulivyoshangaa msikilizaji! Imekuwaje Komora amemsaliti rafiki yake kwa kumvunja moyo kumbe naye alikuwa na mipango ya kujisajili? Jibu ni rahisi, Hofu ya ushindani. Wakati wachezaji hao wakijitambulisha, sio mbali na hapo, Chedede alikuwa katika kiwanja cha mavumbini akijiandaa kumpiga penalti Safina ambaye alikuwa kasimama imara kati ya mawe mawili yalioashiria milingoti ya goli.

**<u>SCENE THREE: DUSTY PLAYGROUND IN TAMBARARE SLUMS</u>**

**38. CHEDEDE:** Natamani Komora angekuwa hapa ajionee, hata sijui aliko.

**39. SAFINA:**Sasa utaipiga hiyo penalti au utaendelea kujigamba?

**40. CHEDEDE:**Niko tayari. Bao la kwanza ndilo hili!

**41.** **SFX: BALL OF PLASTICBAGS BEING KICKED HARD**

**42.** **CHEDEDE: (Screaming out loud)**Ndaniiiii!!!! Nilikwambia hiki ni kitu rahisi sana kwangu, zamu yako.

**43.** **SAFINA:** Uko tayari?

**44.** **CHEDEDE:**Tayari, sijui nifunge macho? **(Giggles)**

**45.** **SFX: BALL KICKED HARD AGAIN**

**46.** **CHEDEDE: (Shocked)** Mungu wangu! Haiwezekani? ...subiri kidogo... umeupigaje mpira?

**47.** **SAFINA:** Moja kwa moja. Kapige penalti ya pili.

**48.** **CHEDEDE: (Angrily)** Sawa, unajifanya stadi sio? Nilikuwa nakuhurumia lakini naona unamea pembe. Wacha nikuonyeshe ngoma. Jaribu kuuzuia huu mkwaju!

**49.** **SFX: BALL KICKED VERY HARD….CAUGHT BY HANDS**

**50.** **SAFINA: (Celebrating)** Hamnaaa!!!!... Nimeokoa penalti, zamu yangu tena.

**51.** **CHEDEDE: (in disbelief)** Haiwezekani! Msichana? Anaokoa penalti? Sina maana tena, mimi ni mchezaji hovyo kabisa! Komora alisema kweli. Kumbe nisingelikubaliwa katika kliniki ya soka..

**52.** **SAFINA:** Kliniki ya soka? Kliniki gani hiyo?

**53.** **CHEDEDE:** Kwani hujui? Metogba anasimamia kliniki ya dimba ili kuiteua timu itakayosafiri hadi Ulaya kushiriki katika mechi za kirafiki.

**54.** **SAFINA: (Excited)** Metogba!? wapi? Tafadhali nipeleke huko. Bado sijayajua vizuri mazingira haya ya mjini.

**55.** **CHEDEDE:** Hapana, huko mahali si kwa watu kama sisi... isitoshe nadhani ulisema shangazi yako atarudi si muda mrefu kutokea sasa?

**56.** **SAFINA:**Ndio lakini hatutakawia, nataka tu kumuona Metogba. Tafadhali... kabla siajasahau naitwa Safina.

**57.** **CHEDEDE:** Mimi ni Chedede, lakini Komora, rafiki yangu huniita Dede.

**58.** **SAFINA:** Sawa Dede, fanya haraka kabla shangazi hajarudi, twende!

**59.** **NARRATOR:** Chedede na Safina, ambao sasa wamekuwa marafiki, waliandamana hadi kwenye uwanja michezo ulio mjini bila kufahamu kilichowasubiri. Wakati huo huo, Jonathan naye alikuwa akiingia uwanjani kavalia jozi ya kilabu moja bingwa na maarufu barani Ulaya.

**SCENE FOUR: SOCCER CLINIC AT THE CITY STADIUM**

**60.** **JONATHAN:** Mkufunzi Metogba... Samahani kwa kuchelewa.

**61.** **METOGBA:** Kwa leo nakusamehe. Lakini usifanye mazoea. **(aloud)** Kila mmoja! Huyu ni…

**62.** **JONATHAN:** Jonathan… Jonathan Makemba.

**63.** **KOMORA:** Makemba? Familia ya Makemba? Mheshimiwa Makemba?

**64.** **METOGBA:** Jonathan ni kijana wa mbunge wenu, lakini hapa sote tuko sawa, ni wa timu moja. Yeye hana tofauti yeyote na wengineo tukiingia uwanjani. Je munafahamu kwa nini ni watu wachache waliojitokeza? Nilitarajia wengi zaidi.

**65.** **KOMORA: (Bit ashamed)** Labda ni kwa sababu vijana wengi wanafanya vibarua mashambani, hapa jijini, na wengine bado wako mwituni.

**66.** **METOGBA:** Mwituni?

**67.** **JONATHAN:** Ana maana kuwa vijana wengine bado wanashirikiana na waasi mwituni, yaani wanatumiwa vitani katika harakati za kuipindua serikali.

**68.** **METOGBA: (takes a deep breath)** Afrika! Lini watoto wataachwa wafurahie utoto wao? Sio neno, tuanze mazoezi. Mizunguko mitano kiwanjani... kasha tukutane katikati. Twendeni! Mbio, mbio!

**69. SFX: WHISTLE BLOWS FOLLOWED BY JOGGING FOOTSTEPS**

**70. <u>OUTRO:</u>**

**70. NARRATOR:** Metogba aligonga ndipo.Vijana wengi sana walio na vipaji wanatumiwa vibaya na wafanyabiashara laghai au wababe wa kivita kuwashambulia raia barani Afrika. Tuwasaidie vipi kuwarejesha katika maisha ya kawaida, ili waweze kuzitimiza ndoto zao? Swali hilo ndilo linalotuhitimishia makala ya leo.Ungana nasi tena wiki ijayo wakati Chedede na Komora watakapokutana ana kwa ana. Jee Safina atafanikiwa kujiunga na timu hiyo? Shangazi yake ataichukulia vipi hatua hiyo? Ukipenda kusikiliza kipindi hiki tena au chengine kilichotangulia tembelea tovuti zetu www.dw world.de/lbe. Mpaka wakati huo, shangilia Afrika!